HOTUBA YA MSTAHIKI MEYA WA MANISPAA YA MOROGORO MHE. PASCAL M. KIHANGA KATIKA MKUTANO WA KAWAIDA WA MWAKA WA BARAZA LA MADIWANI LA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO TAREHE 30/06/2023

Mhe. Naibu Meya,
Waheshimiwa Wabunge,
Waheshimiwa Madiwani,
Mkurugenzi wa Manispaa,
Wakuu wa Divisheni na Vitengo,
Watendaji wote,
Wanahabari,
Ndugu Wananchi,
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana.
Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kufika hapa tukiwa na afya njema. Pia nawakaribisha Wananchi wote mliohudhuria mkutano huu wa leo.

Ninawashukuru Watendaji na Wadau wote wa Halmashauri walioshiriki kwa pamoja kwa namna moja au nyingine katika kuandaa mkutano huu.

Ninawashukuru Wananchi wote kupitia Mabaraza ya Maendeleo ya Kata na katika vikao vilivyofanyika katika nyakati na ngazi mbalimbali. Ninapenda kuwahakikishia kuwa mawazo yenu yamezingatiwa kwa kadiri ilivyowezekana katika uandaaji wa mkutano huu.

Aidha, ninawashukuru wote mliotenga muda wenu leo kuhudhuria Mkutano huu muhimu. Kuwepo kwenu hapa ni kielelezo cha kutambua umuhimu wa kushiriki mkutano huu na kufahamu hali ya utoaji wa huduma na mipango mbalimbali ya maendeleo ya Manispaa yenu.

Napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Madiwani na Watendaji wote wa Halmashauri kwani kutokana na ushirikiano wao tumeweza kutekeleza majukumu mbalimbali kwa ufanisi mkubwa. Ninawashukuru sana.
Ninatambua na ninafurahi sana uwepo wa Waandishi wa habari kwani kupitia kwenu taarifa zitaweza kuwafikia Wananchi ambao hawakuweza kuwa nasi hapa leo. Kwenu wote ninasema ahsanteni sana.

Ninamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze katika kupitia na kutolea maamuzi yote yatakayojadiliwa.

Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi:
Halmashauri kupitia Kamati zake za Kudumu na Baraza la Madiwani imetekeleza azma yake ya kuboresha na kuinua hali ya maisha ya wakazi wa Manispaa ya Morogoro kwa kutoa huduma bora na endelevu za kijamii, kiuchumi na kudumisha utawala bora unaozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu katika kipindi chote cha mwaka wa fedha 2022/2023.

Katika kutekeleza azma hii yapo mafanikio mbalimbali ambayo Halmashauri imeyapata. Utekelezaji na mafanikio hayo umezingatia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) pamoja na Mikakati ya Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA). Mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:-

MAPATO NA MATUMIZI YA HALMASHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Mapato

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ilipokea na kukusanya fedha kwa mwaka 2022/2023 jumla ya **Tshs. 80,823,086,209.00** ambayo ni sawa na asilimia **95** ya makadirio ya **Tsh. 84,561,722,000.00** ya mwaka 2022/2023, kama ifuatavyo:-

- Mapato ya Ndani (Own Source) yalikuwa ni **Tshs. 12,653,562,636.00** ambayo ni sawa na asilimia **100** ya makisio ya **Tshs. 12,654,400,000.00** ya mwaka 2022/2023 kwa mapato ya ndani.
- Miradi ya maendeleo, jumla ya **Tshs. 8,497,409,723.00** zilipokelewa kutoka Serikali Kuu ambazo ni sawa na asilimia **93** ya makisio ya **Tshs. 9,115,045,000.00** ya mwaka wa fedha 2022/2023.
- Mishahara na matumizi mengineyo (OC) jumla ya **Tshs. 59,672,113,849.00** zilipokelewa ambazo ni sawa na asilimia **95** ya makisio ya **Tshs. 62,792,277,000.00**.

Mikakati ya kufikia malengo

Halmashauri ina mikakati mbalimbali ya kukusanya mapato kama ifuatavyo:-

- Kutoa elimu kwa walipa kodi juu ya umuhimu wa kulipa kodi na ushuru kwa ustawi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

- Kuwa na kikosi kazi maalum cha ufuatiliaji wa mapato ambacho kilianza katika eneo la Msamvu na sasa kinaendelea katika vyanzo vingine
- Kutoa elimu kuhusu ulipaji wa kodi mbalimbali kwa wakati kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa Manispaa ya Morogoro.

Matumizi

Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kutumia kiasi cha **Tshs. 84,561,722,000.00** kwa matumizi mbalimbali ikiwemo mishahara, matumizi ya ruzuku, matumizi yasiyo ya ruzuku pamoja na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Juni 2023 Halmashauri ilitumia kiasi cha **Tshs. 77,609,466,521.95** sawa na asilimia **92** kwa mchanganuo ufuatao:-

- Mishahara, matumizi ya ruzuku na matumizi yasiyo ya ruzuku Halmashauri ilitumia kiasi cha **Tshs. 65,561,517,442.17** kati ya **Tshs. 69,769,247,200.00** sawa na asilimia **94** ya makisio.
- Miradi ya maendeleo. Halmashauri ilitumia kiasi **Tshs. 12,047,949,079.78** kati ya **Tshs. 14,792,474,800.00** sawa na asilimia **81** ya makisio.

1.0 DIVISHENI YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi:
Divisheni hii imefanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kumetengwa na kupimwa maeneo ya uwekezaji Kiegea.
- Kuna ongezeko la viwanda vidogo **96** katika Kata za Mkundi, Kingolwira, Lukobe, Mafisa, Kichangani na Kihonda.
- Uanzishwaji wa matumizi ya mfumo mpya wa kukusanyia mapato, urasimishaji wa biashara na utoaji wa leseni unaoitwa **TAUSI**. Mfumo huu unalenga kuongeza uwezo wa kukusanya mapato na kuondoa madeni yaliyokuwa yakijitengeneza kwa mfumo wa zamani.

2.0 DIVISHENI YA AFYA, USTAWI WA JAMII NA LISHE

Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi
Divisheni ya Afya, Ustawi wa Jamii Na Lishe ilipokea fedha kutoka Serikali Kuu na Mapato ya ndani na zilitumika kutekeleza miradi ifuatayo;-

A) FEDHA KUTOKA SERIKALI KUU

i. Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya

Manispaa ilipokea jumla ya **sh. 1,000,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa majengo 4 ambayo ni Wodi ya wazazi, Mionzi, jengo la kufulia na dawa, Majengo yote yapo katika hatua za umaliziaji.

ii. Ujenzi wa wodi ya wazazi Zahanati ya Konga

Manispaa ilipokea kiasi cha **Tsh 50,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wazazi jengo lipo kwenye hatua ya umaliziaji.

B) FEDHA ZA MAPATO YA NDANI

Manispaa ya Morogoro katika mwaka wa fedha 2022/23 imepeleka jumla ya **Tshs. 555,000,000** kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Kituo cha Afya **1** na Zahanati 4 ndani ya Manispaa.

Shughuli zifuatazo zimefanyika katika Sekta ya Afya:-

i. Wigo wa dawa zinazopatikana vituoni umeongezeka kutoka asilimia 96.8 mwaka 2021/2022 mpaka kufikia asilimia 96.91 mwaka 2022/2023.

ii. Katika kipindi cha mwaka 2022/2023 Halmashauri imefanikisha ujenzi wa Zahanati 4 ambazo ni Uwanja wa Taifa, Mazimbu, Mlapakolo na Kiegea B mchakato wa upatikanaji wa vifaa unaendelea kufanyika ili zianze kutoa huduma. Zahanati ya Kauzeni na kituo cha Afya Tungi bado zipo kwenye hatua za umaliziaji .

iii. Katika kipindi cha mwaka 2022/2023 Halmashauri imefanikiwa kufunga mfumo wa " Got homis" katika zahanati 5 ambazo ni Mwembesongo, Malipula, Misongeni, Kilakala na Mjimpya kufanya jumla ya vituo vilivyofungwa mfumo kufikia 10, lengo likiwa ni kusimamia makusanyo ya mapato ya vituo na taarifa za wateja kwa ujumla. Aidha Halmashauri inaendelea kufunga mfumo kwenye vituo vilivyobaki.

iv. Kuongezeka kwa wajawazito waliokuwa wakijifungulia katika vituo vya Afya kutoka asilimia 97 mwaka 2021/2022 hadi asilimia 98.3 mwaka 2022/2023.

v. Halmashauri imeendelea kuzuia maambukizi ya malaria kwa kugawa vyandarua katika Kata 7 zenye maambukizi makubwa ya malaria kwa kina mama wajawazito na watoto chini ya miaka 5. Hivyo kufanya maambukizi ya malaria kupungua kutoka asilimia 5.7 kwa mwaka 2021/2022 kufikia asilimia 5.3 kwa mwaka 2022/2023.

vi. Kiwango cha maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa wateja waliopimwa kimepungua kwa asilimia 3.2 kutoka asilimia 6.6 mwaka 2021/2022 hadi asilimia 3.4 ya mwaka 2022/2023.

vii. Vituo vya huduma vimeongezeka kutoka 80 mwaka 2021/2022 hadi 86 mwaka 2022/2023. Ambapo vituo vya serikali jumla ni 29.

2.2 Huduma ya Chanjo

Katika kuhakikisha jamii inakingwa dhidi ya magonjwa ya mlipuko hususani kwa watoto chni ya miaka 5 elimu ya chanjo imeendelea kutolewa vituoni na huduma za mkoba ziliyohusisha matembezi ya nyumba hadi nyumba.

Kiwango cha utoaji wa chanjo kwa mwaka 2022/2023 tumefikia asilimia 116

Kasi ya uchanjaji imeongezeka kwa kiasi kikubwa katika baadhi ya chanjo ikiwemo, chanjo ya Saratani ya mlango wa kizazi , chanjo ya Uviko 19 na chanjo ya Surua Rubella.

Aidha tunategemea kukamilisha miradi ifuatayo:-

i. Kumalizia ujenzi wa kituo cha Afya Tungi
ii. Kumalizia Majengo ya kituo cha Afya Lukobe(OPD,Maabara,Wodi ya Wazazi na Jengo la Kufuria).
iii. Kumalizia miundombinu ya zahanati 2 ambazo ni Kiegea B (Nyumba ya mtumishi) na Kauzeni.
iv. Uendelezaji ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Mkundi.

2.3 TAARIFA YA AFYA MAZINGIRA (KINGA) MWAKA 2022/2023- MANISPAA YA MOROGORO.

Shughuli zilizofanyika katika Kitengo cha Afya kinga-afya Mazingira kwa mwaka 2022/2023 ni shughuli zote za afya ya jamii zikilenga kuikinga jamii na magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza pamoja na kuhakikisha huduma inayotolewa kwa jamii ni bora na haiathiri Afya ya mtoaji, afya ya mhudumiwa, na afya ya jamii inayozungunga.

Shughuli hizo ni pamoja na ukaguzi wa maeneo yote muhimu ambayo ni tanuri za kuoka mikate (bekari), kwenye viwanda, makanisa, maduka, huduma za vyakula,nyumba za kulala wageni, misikiti, mabenki, nyumba za kuishi, magodown ya vinywaji na vyakula na masoko. Pia kuhamasisha uchanjaji wa chanjo ya uviko na kutoa chanjo ya UVIKO, kusimamia utoaji wa chanjo zingine zinazotolewa kila siku kama vile surua , polio na pepopunda pia kutoa matone ya vitamin A.

2.4 TAARIFA ZA MAGONJWA YA MILIPUKO NA MIKAKATI YA KUZUIA MAGONJWA YA MILIPUKO.

Hakuna magonjwa ya mlipuko yaliyotokea Manispaa ya Morogoro kwa kipindi hiki cha mwaka 2022/2023.

2.5 MIKAKATI JA KUJIKINGA NA MAGONJWA YA MLIPUKO

Manispaa ya Morogoro imepitiwa na barabara kuu kutoka kanda ya ziwa ,kutoka nyanda za juu kusini kuelekea mikoa ya Pwani, Dar es salaam na kuelekea kusini mwa Tanzania. Pia imepitiwa na reli ya kati ikitokea Mwanza/Kigoma kuelekea Dar es salaam.

Kwa kupitiwa na njia hizo inafanya muingiliano wa watu kutoka mikoa mbalimbali kuchanganyikana hapa Manispaa na hivyo kuifanya Manispaa kuwa na hatari ya

kusambaa kwa magonjwa ya mlipuko **kiepidemiolojia** pindi yatokeapo sehemu yoyote ya nchi na hivyo Kitengo cha Afya kimekuwa kikichukua tahadhari kila muda kuzuia magonjwa ya milipuko. Jitihada zinazofanyika ni pamoja na;

1. Kusimamia uwekaji wa vifaa vya kunawia mikono kwenye maeneo ya jumuia na kuhimiza matumizi ya vitakasa mikono.
2. Kutoa elimu ya Afya mashuleni, misikitini, makanisani, kwenye vikao, mikutano, makongamano na vyombo vya habari.
3. Kufanya Ukaguzi kwenye maeneo wanapo kula abiria wa mabasi ya mikoani.
4. Ukaguzi wa nyumba kwa nyumba, maeneo mbalimbali ya biashara na taasisi kufanyiwa ukaguzi wa mara kwa mara na kuchukuwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria. (kuelimisha, kutoa ilani ya marekebisho, kutoza faini inapobidi na kufungia maeneo hatarishi inapobidi)
5. Kuhimiza upimaji wa afya kwa biashara na huduma mbalimbali kwa mujibu wa sheria.

2.6 KUNG'ATWA NA MBWA (WANYAMA)

Katika kipindi cha mwaka 2022/2023, jumla ya watu 187 waling'atwa na mbwa na kati ya hao 103 walipatiwa chanjo ya kichaa cha mbwa baada ya kujiridhisha kuwa na uwezekano mkubwa wa mbwa waliowang'ata walikuwa na kichaa cha mbwana wengine 84 walipatiwa chanjo ya pepopunda baada ya kujiridhisha kuwa mbwa waliowang'ata hawakuwa na uwezekano wa ugonjwa wa wakichaa cha mbwa lakini waliambiwa kwenda kuwaangalia mbwa waliowang'ata kwa siku 10 kama bado wapo hai.. Wagonjwa wengi zaidi walitoka kata ya Kihonda (38)

2.7 MASHINDANO YA USAFI

Manispaa ya Morogoro imekuwa ikitekeleza kampeni ya kitaifa ya usafi wa Mazingirainayoratibiwa na Wizara ya Afya OR-TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kushindanisha mitaa kwa kila kata ili kupata mtaa 1 ulioshinda ambapo mitaa hiyo hushindanishwa ili kupata mtaa safi zaidi kwa Manispaa ambapo mitaa mitano huwakilisha Manispaa kitaifa.

Katika kipindi cha Februari Juni, 2023 michakato ya mashindano ilifanyika kuanzia kata husika hadi manispaa na mitaa iliyoshinda kwa kila kata ni kama ifuatavyo;

MITAA ILIYOSHINDA KWA KILA KATA MWAKA 2023.

NA.	JINA LA MTAA	JINA LA KATA	ALAMA
1	MAZIMBU CAMPUS	MINDU	94
2	BOMA ROAD	MJI MKUU	93
3	BIGWA BARABARANI	BIGWA	92
4	AZIMIO	KIHONDA	86

5	SALUM ABDALLAH	KINGO	83
6	AREA FIVE	KICHANGANI	83
7	BWINILA	KILAKALA	77
8	KINGALU	BOMA	77
9	SABASABA	MBUYUNI	76
10	LITI	MLIMANI	76
11	MGUDENI	LUKOBE	75
12	NYERERE	MAFISA	75
13	NGOMA A	MJI MPYA	73
14	BIMA	K/MAGHOROFAN	72
15	BWAWANI	MKUNDI	72
16	MTONI	MZINGA	71
17	BOMA A	MAZIMBU	71
18	MWEMBENI	CHAMWINO	68
19	MAFIGA B	MAFIGA	68
20	MFURUNI	TUNGI	64
21	KIDIDIMO SUA	MAGADU	64
22	JOHN MAHENGE	SABASABA	64
23	KILALA	LUHUNGO	63
24	GEZAULOLE	KAUZENI	62
25	KIKUNDI	SULTAN AREA	60
26	KIWALANI	K/NDEGE	59
27	JUMAHAMSINI	MWEMBESONGO	54
28	KISWANYA	UWANJA WA TAIFA	54
29	SHULE	KINGOLWIRA	45

MITAA MITANO ILIYOONGOZA KWA MANISPAA MWAKA 2023.

NA.	JINA LA MTAA	JINA LA KATA
1	BOMA ROAD (76%)	MJI MKUU
2	JOHN MAHENGE (73%)	SABASABA
3	MAFIGA B (72%)	MAFIGA
4	AREA FIVE (71%)	KICHANGANI
5	SALUM ABDALLAH (69%)	KINGO

2.8 UPIMAJI WA AFYA

Jumla ya watu 4864 wanaojihusisha na vyakula, viwanda, saluni na kazi za usafi walipima Afya zao ambapo jumla ya shilingi 9,728,000 zilikusanywa.

Marehemu wasio na ndugu

Marehemu wasio na ndugu ni 52 walizikwa katika makaburi ya Kola katika kipiindi cha mwaka 2022/2023, wa kiume 40, wakike 11 na fuvu moja la kichwa liliokotwa 21/3/2023 Bigwa na kuzikwa mwezi April ambapo jinsia yake haikufahamika)

Tiba asili

Usajili wa muda wa waganga wa tiba asili umeshfanyika ambapo waganga 47 wamesajiliwa kwa usajili wa muda na waganga 15 wamepata usajili wa kudumu.

Vituo vya kutolea tiba asili 13 na maduka 26 yalisajiliwa katika kipindi hiki. Pia Ukaguzi wa vituo na maduka 98 ulifanyika kwa kipindi cha mwaka 2022/2023.

MIRADI ILIYOTEKELEZWA KWA FEDHA ZA MAPATO YA NDANI.

3.0 SEKTA YA ELIMU YA SEKONDARI

Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi:

- Manispaa ya Morogoro kupitia fedha za mapato ya ndani ilipokea kiasi cha **Shs. 432,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Utawala kwa jumla ya shule saba kama mchanganuo unavyoonekana;-

Jedwali hapa chini linaonesha mgawanyo wa fedha uliofanyika.

JINA LA MRADI	HALI YA KAZI	KIASI
Ujenzi wa jengo la Utawala Mazimbu	Hatua ya ukamilishaji	50,000,000
Ujenzi wa jengo la Utawala Mbuyuni Modern	Hatua ya ukamilishaji	50,000,000

Ujenzi wa jengo la Utawala Kola	Hatua ya ukamilishaji	50,000,000
Ujenzi wa jengo la Utawala Mkundi Mlimani	Imekamilika	132,000,000
Ujenzi wa jengo la Utawala Mwembesongo	Hatua ya ukamilishaji	50,000,000
Umaliziaji wa jengo la Utawala Mafiga	Imekamilika	50,000,000
Ujenzi wa jengo la Utawala Tungi	Hatua ya ukamilishaji	50,000,000
JUMLA KUU		**432,000,000**

Aidha, Halmashauri ina jumla ya Shule **55**, kati ya hizo **29** ni za Serikali na **26** ni za binafsi. Wanafunzi **36,951** wakiwemo wavulana **17,488** na wasichana **19,463** kati ya Wanafunzi hao, Wanafunzi **28,507** ni wa Shule za Sekondari za Serikali, wakiwemo wavulana **13,456** na wasichana **15,051** na wanafunzi **8,444** ni wa shule za binafsi wakiwemo wavulana **4,032** na wasichana **4,412.**

i) Watumishi wa Divisheni ya Elimu Sekondari

Divisheni ya Elimu Sekondari ina jumla ya Walimu **1,219** wakiwemo wanaume **543** na wanawake **676**. Kati ya Walimu hao, Walimu **352** ni Walimu wa sayansi na hisabati na Walimu **867** ni wa masomo ya sanaa. Aidha Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ina upungufu wa Walimu **105** wa masomo ya hisabati na sayansi.

a) Miundombinu na samani

Divisheni ya Elimu ikishirikiana na Mhandisi wa Manispaa inasimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa, ujenzi wa vyumba vya maabara za sayansi na samani.

b) Miundombinu na Samani

MAHITAJI		**YALIYOPO**	**UPUNGUFU**
Meza	28,507	25,607	3,382
Viti	28,507	25,619	3,425
Nyumba za Walimu	1,219	46	1,173
madarasa	624	582	42

c) Taaluma

Ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha sita mwaka **2022** ni asilimia **99.7**. Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha nne ni asilimia **86.4** mwaka 2022. Jumla wanafunzi **2242** wamechaguliwa kwenda kidato

cha tano mwaka 2023. Kati ya wanafunzi hao, wanafunzi **814** wamechaguliwa tahasusi za sayansi, wanafunzi **1222** wamekwenda tahasusi ya sanaa na wanafunzi **208** wamekwenda tahasusi ya biashara. Hata hivyo wanafunzi **587** wamechaguliwa kwenda vyuo mbalimbali kati ya hao **108** wamechaguliwa kwenda vyuo vya sayansi.

ii) Mikakati ya kukabiliana na changamoto katika elimu ya Sekondari.

Kuendelea kutenga fedha katika bajeti ya kila mwaka ili kujenga na kukarabati miundombinu na samani za shule mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa.Kuwajengea uwezo walimu ili kuinua kiwango cha ufaulu na kuhakikisha tunafuta sifuri. Pia kuwapatia vitabu vya ziada na kiada walimu na wanafunzi, ukamilishaji waa vyumba vya maabara ili kuwahamasisha wanafunzi kupenda masomo ya Sayansi.

4.0 SEKTA YA ELIMU MSINGI

Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi:

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipokea fedha kisi cha **Shs. 2,342,450,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Miundombinu mbalimbali ya shule. Mchanganuo wa mapokezi ya fedha hizo ni kama ilivyo hapa chini:-

- Fedha ya BOOST iliyopokelewa katika shule 10 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya 2, ujenzi wa madarasa **18**, ujenzi wa matundu ya vyoo **63**, ujenzi wa majengo ya Utawala **2** na ununuzi wa samani.
- Ukarabati wa madarasa **15** katika shule kongwe **10** kiasi kilichopokelewa ni **Shs. 180,000,000.00**.
- Ukamilishaji wa madarasa **6** katika shule **6** kiasi kilichopokelewa ni **Shs. 81,250,000.00**
- Ujenzi wa uzio wa wanafunzi wenye mahitaji maalum Shule ya Msingi Kihonda kisi cha **Shs. 30,000,000.00.**
- Ujenzi wa shule mpya ya Jitegemee **Shs. 400,000,000.00.**
- Ujenzi wa shule mpya ya Kihonda Maghorofani **Shs. 250,000,000.00.**

Halmashauri imefanikiwa kuongeza idadi ya Wanafunzi walioandikishwa kuanza darasa la awali na darasa la kwanza.

- **Darasa la awali**
  Wanafunzi waliosajiliwa kuingia darasa la awali mwaka 2023 ni **7,919**, wavulana **4,056** na wasichana **3,863** kwa shule za serikali na binafsi. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia **9.05.**

- **Darasa la kwanza**
  Wanafunzi waliosajiliwa kuingia darasa la kwanza mwaka 2023 ni **12,246** kati yao wavulana **6,180** na wasichana **6,066** kwa shule za serikali na binafsi. Uandikishaji umeongezeka kwa asilimia **4.74**.

- **Mafanikio ya Sekta ya Elimu Msingi:**
  Kumekuwa na ongezeko la miundombinu ikiwemo madarasa, matundu ya vyoo na samani katika shule za msingi kwa kiwango cha kuridhisha. Kwa mfano madarasa yaliyopo ni **826** na mahitaji ni madarasa **1,793** hadi Juni, 2022. Vyoo mahitaji **3233**, yaliyopo **940**.

  Aidha nyumba za walimu zilizopo ni **81** kati ya nyumba **1,966** zinazohitajika Juni, 2022. Pia matundu ya vyoo vya wanafunzi yaliyopo ni **940** ilipofika Juni 2022 na madawati mahitaji ni **23,698** na yaliyopo ni **16,133** ilipofika Juni 2022.

  Kwa upande wa vitabu uwiano kwa wanafunzi umepungua kutoka **1:3** mwaka 2022 hadi **1:2** ilipofika Juni 2022. Hali ya vitabu kwa sasa shuleni kuanzia darasa la I – V inaridhisha. Halmashauri imepata vitabu kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

- **Mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi**
  Waheshimiwa Madiwani Mwaka 2022 mtihani wa kumaliza elimu ya msingi ulifanyika mwezi Oktoba, 2022. Jumla ya watahiniwa **10,525** walisajiliwa ambapo wavulana **5,180** na wasichana **5,345**.
  Ufaulu wa wanafunzi waliomaliza darasa la saba mwaka 2022 ulikuwa ni **asilimia 92.5,** wanafunzi **9,677** walifaulu wakiwemo wavulana **4,702** na wasichana **4,975** kati ya **10,460** waliofanya mtihani wakiwemo wavulana **5,137** na wasichana **5,323** jumla **10,460**.

  Aidha Halmashauri inaendelea kutekeleza agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuhakikisha kuwa kusiwepo na Mwanafunzi anayekaa chini kwa kukosa madawati. Halmashauri kupitia vyanzo vyake

mbalimbali, Serikali Kuu na kushirikiana na Wadau wanaendelea na uchongaji wa madawati kama jedwali lifuatalo linavyoonesha.

	MAHITAJI	**YALIYOPO**	**UPUNGUFU**
Awali	3,586	723	2,686
Msingi (I – VII)	20,570	14,477	6,093
JUMLA	**23,979**	**15,200**	**8,779**

5.0 SEKTA YA UJENZI

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro katika mwaka wa fedha 2022/2023, Divisheni ya Miundombinu, Uendeshaji wa vijijini na Miji ilijikita katika kuboresha miradi mbalimbali katika sekta ya Elimu, Afya na Utawala kama ifuatavyo:-

i) Sekta ya Afya:

- Uendelezaji wa ujenzi wa zahanati ya Kauzeni Kata ya Kauzeni.
- Uendelezaji wa ujenzi wa Zahanati ya Mji Mkuu
- Uendelezaji wa ujenzi wa Kitu cha Afya Tungi.
- Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika Kata ya Kihonda kwa majengo ya Maternity, Radiology, Laundry na Pharmacy.

ii) Sekta ya Elimu:

- Ujenzi wa majengo ya Utawala shule za Sekondari Kolahill, Tungi, Mkundi Mlimani, Mazimbu na Mbuyuni Modern.
- Ujenzi wa darasa la Awali la mfano shule ya msingi Lukobe
- Ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na ofisi pamoja na vyoo matundu ishirini na nne (24) shule ya msingi Msamvu B (TEA)
- Uendelezaji wa ujenzi wa shule ya Sekondari Kata ya Boma
- Umaliziaji wa vyumba vya madarasa shule za Msingi Juhudi, Tubuyu, Mafiga na Bigwa
- Ukarabati wa vyumba vya madarasa shule za Msingi Mwembesongo, Kaloleni, Sabasaba na Mkundi.
- Ujenzi wa shule Mpya tatu (3) za Msingi Kata ya Mafisa, Chamwino na Mindu (vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo) – BOOST
- Ujenzi wa vyumba vya madarasa shule za Msingi Kilongo, Kingolwira, Mazimbu A, Nanenane, Mgolole, Bungo na Muungano- BOOST
- Ujenzi wa mabweni na madarasa shule ya Sekondari Kilakala.

iii) Utawala:

- Ujenzi wa Jengo la Wamachinga eneo la Fire

6.0 SEKTA YA MIPANGO MIJI, ARDHI NA MALIASILI

Waheshimiwa Madiwani Halmashauri inaendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Manispaa (Morogoro Master Plan) ulioidhinishwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mwezi Machi 2021. Mpango huo utasimamia uendelezaji na ukuaji wa mji kwa kipindi cha miaka **20** hadi kufikia mwaka 2036.

Aidha Halmashauri inaendelea kusimamia mpango wa kuendeleza eneo la biashara katikati ya Mji (CBD) unaolekeza ujenzi wa majengo kwenda juu yaani ujenzi wa majengo ya ghorofa ili kuongeza ujazo, maeneo ya huduma katikati ya mji na pia kuboresha muonekano wa mji. Mpangohuu unalenga kuongeza matumizi ya ardhi yenye kuleta tija kulingana na thamani ya ardhi katikati ya mji.

Pia Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro itaendelea kupanga mji, kupima na kumilikisha ardhi kwa Wananchi mbalimbali ili kuweka mpangilio mzuri wa mji na kuhakikisha upatikanaji wa maeneo ya miundombinu na huduma za jamii. Shughuli hii itaendelea kwa kutumia wataalam wa ndani na pia kushirikiana na sekta binafsi kupitia mpango wa urasimishaji wa makazi, upimaji shirikishi na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa njia ya miradi ya ubia.

Katika utekelezaji wake Halmashauri kupitia Wataalam wake wa ndani katika mwaka wa fedha 2022/2023 imeweza kupanga na kupima viwanja **11,911,** katika Shamba la Tungi Sisal Estate, kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 4,000 linalopatikana katika Mtaa wa Kiegea A Kata ya Kihonda na Kiegea B Kata ya Mkundi.
Aidha, kwa kushirikiana na sekta binafsi zaidi **viwanja 6,800** vimepimwa kupitia mpago wa urasimishaji wa makazi katika mitaa mbalimbali ndani ya Halmashauri katika mwaka 2022/2023 na kazi hii inaendelea. Lengo la Halmashauri ni kutokomeza ujenzi holela na kuhakikisha maneo yote yanayorasimishwa yanakamilika katika mwaka 2023/2024. Nitoe wito kwa wananchi wenye uhitaji wa kujenga nyumba kufika Manispaa ili waweze kupata viwanja vilivyopangwa na kupimwa ili kupunguza ujenzi holela kwani viwanja vipo vingi na vinapatikana kwa bei nafuu.

Sanjari na hayo, Halmashauri imeendelea na utatuzi wa migogoro mbalimbali ya ardhi mikubwa na midogo. Utatuzi wa migogoro hiyo umeendelea kufanyika kwa kushirikiana na Viongozi katika ngazi ya Wilaya, Mkoa na hata Kitaifa. Kwa sasa migogoro mikubwa iliyopo inahusu wananchi waliojenga ndani ya msitu wa kuni

(CCT Forest) na Wananchi waliojenga ndani ya hifadhi mita **500** katika bwawa la Mindu

Migogoro hii imepatiwa ufumbuzi ambapo maamuzi ya Baraza la Mawaziri yamekwishatolewa na maelekezo ya Serikali ni kumega eneo la ekari 5113 katika eneo la hifadhi ya msitu wa kuni CCT na kuondoa wananchi waliojenga ndani ya hifadhi ya mita 500 katika Bwawa la Mindu. Aidha wananchi waliojenga ndani ya hifadhi ya mita 500 ya bwawa la Mindu watapatiwa viwanja katika eneo la CCT. Hata hivyo maamuzi ya baraza la Mawaziri katika mgogoro huu yameelekeza mtaa wa CCT kubaki katika Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero

Kuhusu wananchi wenye madai mbalimbali ya viwanja yaliyosababishwa na miliki pandikizi na maamuzi ya Mahakama, Halmashauri imetoa viwanja 1350 kwa wananchi wote waliokuwa na madai na kuhakikiwa uhalali wa madai yao. Nitoe wito kwa wananchi wote ambao walihakikiwa na kuthibitika kuwa na madai kufika katika Ofisi za Ardhi Manispaa kwa ajili ya kukabidhiwa viwanja vyao.

2.0 SEKTA YA UDHIBITI WA TAKA NA USAFISHAJI

Shughuli za usafi wa mji katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 zilifanyika kwa kufanya mambo yafuatayo;

i. Kubinafisisha shughuli za uzoaji wa taka na ukusanyaji wa ada ya taka kwa Kampuni moja na vikundi vya usafi 13. Kampuni ilitoa huduma kwa Kata 12 na masoko 3. Vikundi vilitoa huduma kwa Kata 14.
ii. Kufanya mapitio ya sheria ndogo ya ada za taka inayokidhi gharama za kusafisha mji na kuiwasilisha ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ajili ya kupitishwa na kuanza kutumika.
iii. Kufanya operation za kila mwezi za kuwakamata na kuwatoza faini wanaochafua mazingira na wanaokaidi kulipa ada ya taka.
iv. Kubinafisisha shughuli za usafishaji wa mto Kikundi kwa Jeshi la Magereza.
v. Kubinafisisha shughuli za usafi wa stendi ya mabasi Msamvu kwa mzabuni mmoja.
vi. Kubinafisisha shughuli za usafishaji wa barabara za lami urefu wa kilometa 57.9, mifereji ya maji ya mvua kwa mzabuni mmoja.
vii. Kuendesha dampo kwa kutumia mitambo ya Manispaa.

3.0 KUHUSU UTAWALA BORA:

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imeendelea kusimamia matumizi ya misingi ya utawala bora ambayo ni utawala wa kidemokrasia, ushirikishwaji wa Umma, utawala wa sheria, haki na usawa kwa watu wote, uwazi katika kuendesha shughuli za maendeleo, uwajibikaji katika utendaji na uadilifu.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri imeshuhudia kuongezeka kwa uwajibikaji miongoni mwa Watumishi wa Umma, kupungua kwa malalamiko yanayohusiana na utoaji huduma, vikao na mikutano kuendeshwa kwa mujibu wa ratiba na kuongezeka kwa ushiriki wa wananchi katika mikutano hiyo.

i) Upandishaji vyeo Watumishi

Baada ya Serikali ya awamu ya sita kuidhinisha upandishaji vyeo watumishi nchini, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro katika Ikama na Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 imewapandisha vyeo jumla ya watumishi 1,042 kwa mchanganuo ufuatao:-

- Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi watumishi 488
- Divisheni ya Elimu Sekondari watumishi 394
- Divisheni ya Afya, Ustawi wa Jamii na Huduma za Lishe watumishi 70
- Divisheni ya Rasilimali Watu na Utawala watumishi 53
- Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi watumishi 16
- Divisheni ya Maendeleo ya Jamii watumishi 12
- Divisheni ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji watumishi 4
- Divisheni ya Miundombinu, Uendelezaji wa Vijiji na Miji mtumishi 1
- Divisheni ya Mipango na Uratibu mtumishi 1
- Kitengo cha Fedha na Uhasibu watumishi 2
- Kitengo cha TEHAMA mtumishi 1

Jumla 1,042

ii) Ubadilishaji Kada/vyeo watumishi

Jumla ya Watumishi 34 wamebadilishwa kada/vyeo baada ya kujiendeleza kitaaluma.

iii) Ajira Mpya

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri yetu ya Manispaa ya Morogoro imefanikiwa kuajiri jumla ya watumishi wa Ajira Mpya 105 wa kada mbalimbali ikiwemo sekta ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Utawala, Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na Elimu ya Msingi na Sekondari. Hii ni baada ya kupatiwa vibali vya Ajira na Serikali ili kujaza nafasi wazi zilizopo.

ii) Ziara ya mafunzo:

Baraza la Madiwani na Wataalam wa Halmashauri katika mwaka wa fedha 2022/2023 walifanya ziara kwenda Zanzibar katika Baraza la Manispaa Mjini Zanzibar kuanzia tarehe 16 – 19/03/2023 kwa lengo la kujifunza yafuatayo:-

i) Usafi wa mazingira
ii) Upimaji wa viwanja na mipangomiji
iii) Uwekezaji wa vivutio vya kitalii

4.0 MAPAMBANO DHIDI YA VVU NA UKIMWI

Kwa kuzingatia ujumbe wa mapambano dhidi ya UKIMWI wenye kauli mbiu Tanzania bila maambukizi mapya, unyanyapaa na vifo vitokanavyo na UKIMWI inawezekana.

Halmashauri ina idadi ya vituo 80 vinavyotoa huduma ya upimaji wa VVU. Kwa kipindi cha Julai 2022-Juni 2023, kiwango cha maambukizi kilikuwa asilimia **3.4**

Idadi ya watu waliopima VVU kwa kipindi cha Julai 2022-Juni 2023, jumla walikuwa **72,400** wakiwemo wanaume **24,938** na wanawake **47,462** jumla ya waliokutwa na maambukizi ni **2,358** wanaume walikuwa **734** na wanawake walikuwa **1,624.**

Kiwango cha maambukizi ya VVU kwa wateja waliopima kimepungua kwa asilimia 3.2 kutoka asilimia 6.6 mwaka 2021/2022 hadi asilimia 3.4 ya mwaka 2022/2023

Mkakati wa Kimataifa wa kupambana na VVU na UKIMWI ifikapo 2025 (95, 95, 95)

i) **Asilimia 95** ya Jamii wawe wanajua hali yao ya maambukizi kwa kupitia upimaji wa VVU ifikapo 2025
ii) **Asilimia 95** ya watu wote waliopimwa na kukutwa na maambukizi wanaanzishiwa dawa za kufubaza makali ya VVU (ART) ifikapo 2025
iii) **Asilimia 95** ya watu wote walioanzishiwa ART kuhakikisha kuwa kiwango kinapungua kwa kiasi kikubwa ifikapo 2025.
iv) Kushirikiana na wadau mbali mbali wanaojishughulisha na mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI
v) Kuhakikisha kuwa Konga ya watu wanaoishi na VVU na UKIMWI Manispaa ya Morogoro inaendelea kupatiwa elimu ya kuhamasisha kushawishi wenzao na wananchi kupima afya zao na kufanya shughuli mbalimbali za ujasiriamali

5.0 SEKTA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

Divisheni hii inazo Seksheni kuu tatu amabzo ni Seksheni ya Kilimo na Ushirika na Seksheni ya Mifugo na Uvuvi ambazo kwa kipindi chote cha mwaka 2022/2023 kimetekeleza shughuli mbali mbali zilivyo orodheshwa;-

5.1 SEHEMU YA KILIMO NA USHIRIKA

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Sekta ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika imetekeleza shughuli zifuatazo:-

i) Kuendeleza ushirika kwa kufanya ukaguzi katika vyama vya Ushirika **15** kati ya vyama **63,** kutoa elimu ya ushirika katika vyama **20** kati **63,** kusimamia mikutano mikuu katika vyama **15** kati ya vyama **63,** kusimamia mikutano ya bodi **15** kati vyama **63.**

ii) Uhamasishaji wa vikundi **5** na kuongeza vyama vya ushirika kutoka **63** hadi **68** katika mwaka wa fedha 2021/2022.

iii) Kusimamia huduma za ugani kwa kutoa ushauri wa kilimo bora kwa Wakulima **5534** kati ya **8,595** katika mwaka wa fedha 2022/2023

iv) Kusimamia mashamba darasa **5** ya migomba na mashamba **15** ya mfano ya nafaka chini ya sekta binafsi na **10** ya mboga na matunda ya Halmashauri.

v) Kusimamia na kufuatilia upatikanaji wa mbolea mbalimbali ikiwemo mbolea za kuuzia na kupandia (**DAP** & **UREA**). Mbolea inauzwa kwa bei ya ruzuku ambapo **DAP na UREA** kwa mfuko wa kilo 50 ni Tshs.70,000.00.

vi) Kusajili Wakulima **5,534** kati ya **8,595** ambayo ni sawa na **asilimia 64.39** kupitia mfumo wa mbolea za ruzuku na zoezi la kusajili linaendelea kwa msimu wa kilimo ujao.

5.2 SEKSHENI YA MIFUGO

Katika kipindi cha mwaka wa fedha **2022/2023** sekta ya Mifugo imetekeleza shughuli zifuatazo:

i) Ufugaji bora

Jumla ya wafugaji **21,423** wakiwemo wafugaji wa kuku **6,173** na wafugaji wa ng'ombe na mifugo mingine **10,912** kutoka Kata mbalimbali za Manispaa ya Morogoro walipatiwa mafunzo ya kanuni bora za ufugaji.

ii) Usindikaji

Jumla ya wadau **741** walipatiwa elimu ya maziwa ikiwa ni pamoja na utunzaji na uhifadhi bora wa maziwa, usafirishaji mzuri wa maziwa na usindikaji wa maziwa.

iii) Uboreshaji wa Koosafu

Katika kutimiza lengo la kuboresha Koosafu za ng'ombe wa maziwa na kuongeza tija ya uzalishaji wa maziwa, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa kushirikiana na sekta binafsi ilitoa mafunzo ya uhimilishaji (Artificial insermination) kwa jumla ya wafugaji **603** kutoka Kata zote za Manispaa ya Morogoro. Aidha hadi sasa jumla ya ng'ombe **1200** wamehimilishwa kwa kushirikiana na sekta binafsi.

iv) Uzalishaji na hifadhi ya malisho

Mafunzo ya utunzaji nyanda za malisho na uzalishaji wa malisho ya mifugo yalifanyika kwa wafugaji **328** kutoka sehemu mbalimbali za Manispaa ya Morogoro.

v) Mlipuko wa ugonjwa wa homa ya Nguruwe

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Manispaa ilikumbwa na mlipuko wa ugonjwa wa homa ya nguruwe ambapo nguruwe **65** walikufa na **159** waliougua ugonjwa huo walichinjwa. Aidha tulifanikiwa kuudhibiti ugonjwa huo baada ya siku 15 tangu kutokea kwa mlipuko.

vi) Idadi ya Mifugo iliyouzwa na iliyochinjwa

Mifugo iliyouzwa			**Mifugo iliyochinjwa**		
Ng'ombe	Mbuzi/kondoo	Nguruwe	Ng'ombe	Mbuzi/kondoo	Nguruwe
36,123	1,614	1,250	34,275	6,752	2,749

- **Utoaji wa chanjo kwa mifugo**

  Aina na idadi ya mifugo iliyochanjwa dhidi ya magonjwa mbalimbali ya mifugo ni kama ifuatavyo:-

Aina ya mifugo	**Idadi ya mifugo iliyochanjwa**	**Ugonjwa**
Ng'ombe	2,365	HOMA YA MAPAFU
Ng'ombe	2,081	KIMETA
Ng'ombe	1,714	MAPELE NGOZI
Ng'ombe	1,238	BLACK
Ng'ombe	4,06	NDOROBO
Mbuzi	2,015	HOMA YA MAPAFU
Mbwa	4,548	KICHAA CHA MBWA
Mbwa	104	KUHARISHA DAMU
Paka	165	KICHAA CHA MBWA
Kuku	1,082,843	MDONDE
Kuku	1,092,242	GUMBORO
Kuku	1,640,470	NDUI

Seksheni ya Mifugo imeendelea kutumia mitego **3** katika juhudi za kukamata mbwa wanaozurura ili kudhibiti mbwa hao. Jumla ya mbwa **207** wamekamatwa kwa kutumia mitego hiyo na kupumzishwa.

5.3 SEKSHENI YA UVUVI

Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2023 sekesheni ya uvuvi imetekeleza shughuli zifuatazo

i) Mafunzo ya ufugaji wa samaki yalitolewa kwa wadau **2,737** kutoka maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Morogoro.

ii) Jumla ya mabwawa 19 ya kufugia samaki yalianzishwa na watu binafsi katika maeneo mbalimbali kama vile Mazimbu, Mzinga, Boma, kauzen, Kingolwira na Kihonda.

6.0 SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Halmashauri imetoa mikopo yenye thamani ya **Tshs. 323,005,000.00** kwa vikundi **30** ambapo kiasi cha **Tshs. 230,205,000.00** zimetolewa kwa vikundi **23** vya Wanawake na **Tshs. 80,800,000.00** kwa vikundi **05** vya vijana na **Tshs. 12,000,000.00** kwa vikundi **02** vya wenye Ulemavu.

Divisheni imeendelea kuhamasisha uundaji na usajili wa vikundi ambapo jumla ya vikundi **53** vya huduma ndogo ya kifedha vimesajiliwa na kufanya jumla ya vikundi hivyo kufikia **506**. Pia vikundi **293** vya kijamii vimepata usajili hivyo kufanya vikundi vilivyosajiliwa kuwa **3209.**

Divisheni imeweza kuhamasisha jamii kujiunga na mfuko wa Jamii ulioboreshwa ambapo jumla ya Kaya **1,649** zenye wanufaika **8,897** zimeandikishwa na kuingiza kiasi cha **Tshs. 49,470,000.00.**

7.0 MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI (TASAF III (II)

Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi:

Manispaa yetu ni miongoni mwa Halmashauri **186** zinazotekeleza TASAF awamu ya tatu sehemu ya pili kupitia Mpango wa kunusuru Kaya maskini, wenye malengo ya kuwezesha kaya za walengwa kutumia fursa za kuongeza kipato, huduma za jamii na kuwekeza katika kuendeleza watoto wao pia kuwezesha kaya maskini

kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu na msisitizo mkubwa ukiwa katika mambo yafuatayo:-

i) Kuwezesha kaya kufanya kazi na kuongeza kipato;
ii) Kuwezesha kaya za walengwa kuongeza rasilimali zalishi na kuongeza vitega uchumi;
iii) Kuwekeza katika watoto ili kuleta matokeo chanya yatakayodumu kwa muda mrefu;
iv) Kuboresha upatikanaji wa huduma za maji, afya na elimu;
v) Kukuza uchumi wa eneo unakofanyika utekelezaji kutokana na matokeo ya Mpango.

Kuanzia Julai 2022 hadi Juni, 2023 Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ina jumla ya walengwa **3,550** kutoka katika Mitaa **258** kwa Kata zote **29** inayotekeleza mpango wa kunusuru Kaya masikini (TASAF III).

(a) Uhawilishaji fedha kwa Kaya Maskini Mafanikio:-

i) Kupitia Mpango wa TASAF kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Manispaa ya Morogoro ilipokea jumla ya shilingi **778,713,935.00** kutoka TASAF makao makuu na kufanya uhawilishaji kwa Walengwa wa kaya Maskini **3,550** moja kwa moja haya ni malipo ya vipindi vinne tu vya malipo Julai, 2022 - Februari, 2023.

ii) Walengwa wa Mpango wameweza kukuza kipato cha familia na kuwa na uwezo wa kupata milo mitatu kwa siku Walengwa **1,937** waliotembelewa walithibitisha.

iii) Walengwa **251** kutoka mitaa mbalimbali ya mpango walihojiwa kupitia ruzuku wameweza kupata fedha ambazo zinawasaidia kulima mashamba ya mahindi na Alizeti.

iv) Kupitia ruzuku hii kuna walengwa takribani **2005** sawa na asilimia **56** wameweza kuanzisha biashara ndogo ndogo za kuuza ndizi, magenge, ufugaji wa mifugo kama Mbuzi, Nguruwe n.k.

v) Walengwa **1,602** (me **39** na ke **1,602**) wameweza kuunda vikundi **132** na kujiwekea akiba ya **Tsh.21,810,800.00** kupitia utaratibu wa kuweka na kuwekeza na wanakopeshana wao kwa wao, hivyo wameweza kukuza uchumi wa kaya kwa kuendesha miradi/biashara ndogondogo.

vi) Pia Walengwa wameweza kuongeza uwezo wa kuhudumia mahitaji ya shul kwa watoto wao kama madaftari, sare za shule na mahitaji mengine y msingi

vii) **Miradi ya muda (PWP)**
Jumla ya miradi **73** kutoka sekta za miundombinu (ujenzi) maji na mazingir yenye gharama ya **Sh. 150,180,000.00** iliibuliwa na miradi **72** ipo katik utekelezaji na mradi **1** umekwisha kamilika na umekabidhiwa katika serika ya Mtaa wa Mindu.

viii) **Miradi ya Miundombinu**
Manispaa ya Morogoro tarehe 15/05/2023 ilipokea jumla ya **Sh 203,896,819.00** kwa ajili ya ujenzi wa Bwalo la Wazee. Utekelezaji up katika hatua za awali za uandaaji jamii (ushirikishwaji wa jamii) ili wawez kusimamia utekelezaji wa mradi.

Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi:
Nawashukuru kwa kunisikiliza na napenda kutamka kuwa Mkutano hu nimeufungua rasmi.

.....

Mhe. Pascal M. Kihanga,
MEYA WA MANISPAA,
MOROGORO